

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA
DAWA ZA KULEVYA**

TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA

YA MWAKA 2018

YALIYOMO

YALIYOMO	i
ORODHA YA MAJEDWALI	iii
ORODHA YA VIELELEZO	iv
MAELEZO YA WAZIRI	v
DIBAJI	vi
FAHARASA	vii
SURA YA KWANZA	1
1 TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI.....	1
Utangulizi.....	1
Matumizi na uzalishaji wa dawa za kulevya duniani.....	1
Matumizi mabaya ya dawa tiba zenye asili ya Kulevya.....	4
Ukamataji wa dawa za kulevya duniani.....	5
Udhibiti wa biashara ya dawa za kulevya mtandaoni.....	5
Makundi maalum yanayojihusisha na dawa za kulevya.....	5
Matumizi ya dawa za kulevya kwa wanawake.....	5
Wanawake na biashara ya dawa za kulevya.....	6
Wafungwa na matumizi ya dawa za kulevya.....	6
Matibabu kwa waraibu.....	7
SURA YA PILI.....	8
2 UDHIBITI NA MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA NCHINI	8
Utangulizi	8
Kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya.....	8
Mwenendo wa Biashara ya dawa za kulevya nchini.....	8
Udhibiti wa Kemikali bashirifu na Dawa tiba zenye asili ya kulevya.....	16
Udhibiti wa Kemikali bashirifu kupitia mfumo wa kielektroniki	16
Uteketezaji wa dawa za kulevya.....	17
Kesi za dawa za kulevya.....	17
SURA YA TATU.....	19
3 KUPUNGUZA UHITAJI (MATUMIZI) NA MADHARA YANAYOSABISHWA NA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA.....	19
Tatizo la Uhitaji (matumizi) wa dawa za kulevya nchini.....	19
Sababu zinazochangia matumizi ya dawa za kulevya.....	19
Madhara yanayosababishwa na matumizi na biashara ya dawa za kulevya.....	19

Kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya	21
Kupunguza madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya.....	22
Tiba ya methadone	22
Kuwaandaa waraibu kuanza kutumia methadone.....	23
Huduma ya upataji nafuu kwa watumiaji wa dawa za kulevya (Sober House)	23
SURA YA NNE.....	25
4 CHANGAMOTO, HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA MIPANGO YA BAADAYE	25
Changamoto na hatua zilizochukuliwa	25
Mipango ya baadaye.....	26

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2008-2018	10
Jedwali Na. 2: Idadi ya watuhumiwa wa Bangi na Mirungi waliokamatwa kati ya mwaka 2008-2018	12
Jedwali Na. 3: Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2008-2018	13
Jedwali Na. 4: Idadi ya watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa nchini kati ya Mwaka 2008 - 2018.....	14
Jedwali Na. 5: Kesi zilizofikishwa mahakamani mwaka 2018	17
Jedwali Na. 6: Watuhumiwa waliofikishwa mahakamani mwezi Januari - Desemba, 2018.....	18
Jedwali Na. 7: Waraibu Waliopata Huduma ya Methadone Tangu 2011 - 2018.....	23

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2008 - 2018	11
Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa idadi ya watuhumiwa waliokamatwa kwa kujihusisha na Bangi na Mirungi nchini kati ya Mwaka 2008 - 2018	12
Kielelezo Na. 3: Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2008 - 2018 ...	13
Kielelezo Na. 4: Mwenendo wa kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2008 - 2018.....	14
Kielelezo Na. 5: Idadi ya watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa nchini kati ya Mwaka 2008 - 2018	15
Kielelezo Na. 6: Mwenendo wa idadi ya watuhumiwa waliokamatwa wakijihusisha na Heroin na Cocaine kati ya Mwaka 2008 - 2018.....	15

MAELEZO YA WAZIRI

Biashara na Matumizi ya Dawa za Kulevya ni tatizo linaloongezeka si hapa nchini kwetu tu bali duniani kote. Katika kukabiliana na tatizo hili Mhe. Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli akifungua rasmi Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma, tarehe 20 Novemba, 2015 aliahidi kushughulikia mitandao ya wafanyabiashara wakubwa wanaojihusisha na dawa za kulevya bila ajizi.

Vilevile, ilani ya uchaguzi ya CCM 2015-2020, Ibara za 146(vi) na 155(a) - (d) inasisitiza kuimarisha udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya ambazo zinatishia usalama wa nchi yetu na ustawi wa Taifa letu kwa ujumla.

Katika kutekeleza ilani ya CCM na maagizo ya Mhe. Rais Serikali kwa kushirikiana na Taasisi za Kimataifa zimefanikiwa kudhoofisha mitandao ya kihalifu ya biashara ya dawa za kulevya nchini na kupunguza kwa kiasi kikubwa dawa za kulevya zilizokuwa zinaingizwa nchini. Kwa mujibu wa Shirika la UNODC, nchi yetu ilifanikiwa kupunguza uingizaji wa dawa ya kulevya aina ya Heroin kwa asilimia 90.

Aidha, serikali katika jitihada za kuendelea kuimarisha mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya itaendelea kuboresha sheria na kanuni za udhibiti dawa za kulevya pamoja na kutoa miongozo mbalimbali ambayo itaongeza tija na ufanisi.

Serikali, itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ikiwemo taasisi, za kimataifa, katika kuridhia na kutekeleza mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa katika kufanikisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya.



Jenista Joakim Mhagama (Mb)
Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu
(Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu)

DIBAJI

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2018 imeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 60 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015, kama ilivyorekebisha na Sheria Na. 15 ya mwaka 2017 kinachoielekeza Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuandaa na kuiwasilisha bungeni kila mwaka. Lengo likiwa ni pamoja na kuwafahamisha wananchi tatizo la dawa za kulevya na jitihada zilizofanywa na Serikali pamoja na Taasisi zake katika kukabiliwa nalo kwa mwaka 2018. Aidha, Taarifa ya Hali ya Dawa za kulevya Duniani 2018 na 2019 (World Drug Report (2018- 2019) na Taarifa ya Polisi ya hali ya uhalifu nchini 2018 zimetumika kuandaa taarifa hii.

Taarifa hii imegawanyika katika sura kuu nne. Sura ya kwanza inaelezea hali ya tatizo la dawa za kulevya duniani. Sura ya pili imejikita katika tatizo la dawa za kulevya nchini zikiwemo jitihada na mafanikio yaliyopatikana. Sura ya tatu inaainisha tatizo la matumizi ya dawa za kulevya nchini pamoja na jitihada zilizofanyika kudhibiti madhara yatokanayo na matumizi ya dawa hizo.

Sura ya nne inakamilisha taarifa hii kwa kuainisha changamoto, hatua zilizochukuliwa na mipango ya baadaye katika udhibiti na mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya nchini kwa mwaka 2018.

Mwisho, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wadau wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha taarifa hii.



JAMES WILBERT KAJI
KAIMU KAMISHNA JENERALI
MAMLAKA YA KUDHIBITI NA
KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

FAHARASA

ATS	Amphetamine Type Stimulants
LSD	Lysergic Acid Diethylamide
MDMA	3, 4-methylene-dioxy-methamphetamine
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
UNODC	United Nations Office on Drugs and Crime
VVU	Virusi Vya Ukimwi
WHO	World Health Organization
MKIKUTE	Mapambano ya Kifua Kikuu na Ukimwi Temeke.

SURA YA KWANZA

1 TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI

Utangulizi

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2019 inaonesha matumizi ya dawa za kulevya yamekithiri na vifo vinavyotokana na matumizi ya dawa za kulevya vimeongezeka. Takribani watu milioni 271 duniani ambao ni kama 5.5% ya watu wote duniani wenye umri kati ya miaka 15-64 walitumia dawa za kulevya angalau mara moja mwaka 2017. Watu milioni 35 wanaotumia dawa za kulevya wameathiriwa na dawa hizo kiasi cha kuhitaji matibabu. Takribani watu 585,000 walifariki mwaka 2017 kutokana na matumizi ya dawa za kulevya kulingana taarifa ya Shirika la Afya Duniani. Vifo hivyo vilisababishwa na kuzidisha kiwango cha matumizi (overdose), UKIMWI na homa ya ini. Karibu nusu ya vifo hivyo vilitokana na homa ya ini aina C. Takwimu zinaonesha kuwa watumiaji wa dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga wameathirika zaidi.

Dawa za kulevya jamii ya afyuni (opioids) zimeendelea kuongoza kwa kusababisha madhara makubwa zikiwa na 76% ya vifo vilivyosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya. Hali hii inahitaji nguvu ya pamoja kuwezesha juhudi za kuzuia matumizi na kutoa tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevya pamoja na kutoa huduma zinazolenga kupunguza athari za kiafya kwa kuzingatia malengo ya maeneleo endelevu.

Matumizi na uzalishaji wa dawa za kulevya duniani Bangi

Bangi ni dawa ya kulevya iliyotumika zaidi duniani kwa kuwa na watumiaji wanaokadiriwa kufikia milioni 188 katika mwaka 2017 ambao ni sawa na 3.8% ya watu wote duniani wenye umri kati ya miaka 15-64. Katika muongo inaoishia mwaka 2017, watumiaji wa bangi duniani wameendelea kuongezeka na kufikia 16%. Matumizi ya bangi yameendelea kuwa juu katika maeneo ya Afrika Magharibi na Kati (10.0%), Amerika ya Kaskazini (13.8 %) na Oceania (10.9%).

Makadirio yaliyofanywa kwa mara ya kwanza na UNODC mwaka 2016 kutoka nchi 130, yanaashiria kwamba watu milioni 13.8 ambao wengi wao ni wanafunzi wenye umri wa miaka 15-16 walitumia bangi angalau mara moja katika kipindi cha miezi sita ambayo ni sawa na 5.6% ya watu wote wa umri huo. Matumizi ya bangi kwa mwaka katika kundi la umri wa miaka 15-16 yalikuwa juu zaidi ukilinganisha kundi kubwa la umri wa miaka 15-64 (3.9%) katika mwaka 2016.

Bangi hutumika sambamba na dawa nyingine za kulevya na mara nyingi watumiaji wa dawa nyingine huanza na bangi kabla ya kuhamia kwenye dawa nyingine. Baadhi ya nchi zimeruhusu matumizi ya bangi, mfano tangu mwaka 2017 majimbo nane ya Marekani yameruhusu matumizi ya bangi licha ya jimbo la Colorado lililoruhusu kabla. Hata hivyo, kumekuwa na ongezeko la watu wanaohitaji tiba kutokana na matumizi ya bangi. Pia

kumekuwa na ongezeko la vifo vinavyotokana na ajali zinazosababishwa na matumizi ya bangi katika jimbo la Colorado.

Pamoja na kuwa dawa inayotumika zaidi duniani, bangi imeendelea kuwa dawa inayoongoza kwa uzalishwaji katika sehemu nyingi. Katika kipindi cha mwaka 2010–2016, UNODC ilipokea taarifa kutoka nchi 145 juu ya kilimo cha bangi ikiwa ni zaidi ya mara mbili ya nchi zilizotoa taarifa ya kilimo cha mimea ya afyuni (opium poppy cultivation).

Dawa za kulevya jamii ya afyuni (opioids)

Dawa za jamii ya afyuni zimegawanyika katika makundi matatu, kundi la kwanza huhusisha dawa za asili za heroin, morphine, codeine na thebaine ambazo zinatokana na utomvu wa afyuni (opium); kundi la pili ni oxymorphone, hydrocodone, oxycodone na hydromorphone zitokanazo na uchakataji wa codeine na morphine pamoja na kundi la tatu la dawa zinazotengenezwa za methadone, tramadol, fentanyl na meperidine.

Pamoja na kwamba bangi inaongoza kwa matumizi duniani, dawa jamii ya afyuni zinaongoza kwa madhara kwa watumiaji. Mfano 76% ya vifo vilivyotokana na matumizi ya dawa za kulevya mwaka 2015, vilisababishwa na matumizi ya dawa za kulevya jamii ya afyuni. Mwaka 2016 heroin na dawa tiba zinazotumika vibaya ziliongoza kwa kusababisha vifo vingi kutokana na kuzidisha kiasi cha matumizi (overdose). Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2018, wajidunga wa dawa za kulevya wanaokaribia kufikia milioni 10.6 duniani wanapata madhara zaidi kwani katika mwaka 2017 zaidi ya nusu walikuwa na maambukizi ya virusi vya homa ya ini aina C na mmoja kati ya wajidunga wanane alikuwa na maambukizi ya VVU.

Uzalishaji wa utomvu wa afyuni (opium) duniani umepanda kwa 65% katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2017 kwa kiasi cha tani 10,500. Kiwango hiki ni kikubwa kuwahi kurekodiwa na UNODC tangu ianze ufuatiliaji wa uzalishaji wa afyuni mwanzoni mwa karne ya 21. Eneo linalolimwa mimea ya afyuni (opium poppy) duniani limeongezeka maradufu tangu mwaka 2006 kufikia takribani hekta 418,000 mwaka 2017. Ongezeko hili linatokana na ongezeko la kilimo cha mimea ya afyuni (opium poppy) nchini Afghanistan ambayo ilizalisha 86% ya afyuni yote duniani mwaka 2017.

Ongezeko la uzalishaji afyuni nchini Afghanistan lilifikia tani 9,000 mwaka 2017 likiwa ni ongezeko la 85% ikilinganishwa na mwaka mmoja kabla. Ongezeko hilo lilisababishwa na ukosefu wa usalama, rushwa, kukosekana kwa udhibiti wa serikali na ukosefu wa fursa za kiuchumi hivyo kuziacha jamii za vijijini katika hatari ya kushawishiwa na makundi ya biashara ya dawa za kulevya.

Dawa za kulevya za jamii ya Amfetamini (ATS)

Kundi hili huhusisha dawa za kutengenezwa katika maabara haramu zikiwa katika umbo la vidonge au mawemawe kama metamfetamini, amfetamini na MDMA ambayo inafahamika zaidi kama “ecstasy”. Metamfetamini inapatikana zaidi katika nchi za Mashariki mwa Bara la Asia. Masoko ya metamfetamini yameendelea kukua wakati maeneo ya Mashariki na Kusini

mwa Asia pamoja na Amerika ya Kaskazini yameendelea kuongoza kwa biashara ya metamfetamini ulimwenguni. Amerika ya Kaskazini iliripoti kuongezeka kwa upatikanaji wa metamfetamini katika kipindi cha mwaka 2013 na 2016. Mwaka 2016 metamfetamini ilikuwa ni dawa tishio ya pili baada ya heroin nchini Marekani. Kutokana na tafiti mbalimbali kulikuwa na ongezeko la soko la metamfetamini mashariki na kusini mwa Asia pamoja na Oceania, ambako matumizi ya metamfetamini hasa metamfetamini ya mawemawe limekuwa ni tatizo.

Kwa miaka mingi, amfetamini ilikuwa inaongoza kwa upatikanaji katika dawa za kutengenezwa barani Ulaya lakini hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la kiasi kilichokamatwa katika mabara ya Amerika kuashiria ongezeko la biashara hiyo. Takribani watu milioni 34.2 duniani ambao ni 0.7% ya watu wenye umri wa miaka 15–64 walitumia dawa za kulevya jamii ya amfetamini. Watumiaji wengi walikuwa Amerika ya Kaskazini (2.0%), ikifuatiwa ba Oceania (1.3%). Pia matumizi ya “Ecstasy” yanapanuka katika maeneo mengine ya Ulaya Magharibi na Ulaya ya Kati pamoja na Amerika ya Kusini.

Dawa za jamii ya amfetamini zimekuwa zikifuatia kwa kusababisha madhara mengi ya kiafya baada ya zile za jamii ya afyuni. Katika dawa za jamii ya amfetamini, metamfetamini iliongoza kwa kuwa na waraibu wengi wa dawa hiyo waliokuwa wanahitaji tiba. Metamfetamini imekuwa ikutumika zaidi Asia Mashariki na Oceania na imeanza kuenea Amerika ya Kaskazini, Kusini Mashariki mwa Asia na baadhi ya maeneo ya Bara la Ulaya.

Cocaine

Cocaine ambayo hutokana na mmea wa coca hulimwa katika mabara ya Amerika ambako kiasi kinacholimwa kimeongezeka kwa kiasi kikubwa. Kwa mwaka 2017 uzalishaji ulifikia tani 1976 ambayo ni ongezeko la 25% ukilinganisha na mwaka 2016. Ongezeko hilo linachangiwa na ongezeko la uzalishaji nchini Colombia ambayo inazalisha 70% ya cocaine yote Duniani.

Mabara ya Afrika and Asia yamejitokeza kuwa vituo vya usafirishaji na matumizi ya cocaine. Kulikuwa na ongezeko la ukamataji mkubwa wa cocaine mwaka 2016 katika mabara ya Asia na Afrika, ukiashiria kupanuka kwa soko na matumizi ya cocaine.

Kiasi cha cocaine kilichokamatwa Afrika kiliongezeka mara mbili mwaka 2016, kwa nchi za Afrika ya Kaskazini zikiwa na ongezeko la mara sita zikiwa na 69% ya cocaine yote iliyokamatwa eneo la Afrika mwaka 2016. Hii ni tofauti na miaka ya nyuma ambapo cocaine ilikuwa ikikamatwa Afrika Magharibi na Kati.

Dawa mpya za kulevya (NPS)

Katika miaka ya karibuni kumekuwa na ongezeko la dawa mpya za kulevya zisizodhibitiwa na mikataba ya kimataifa. Watengenezaji huiga kemikali zilizoko kwenye dawa za kulevya zinazodhibitiwa kimataifa kama bangi, cocaine, heroin na metamfetamini. UNODC ilipokea taarifa ya dawa mpya za kulevya zipatazo 803 katika kipindi cha mwaka 2009–2017.

Kati ya dawa hizo, dawa mpya aina ya fentanyl na jamii zake inaongoza kwa kuleta madhara kwa watumiaji. Uzalishaji wa dawa unaongezeka kwa kiwango kikubwa kutoka jamii moja mwaka 2009 mpaka jamii 46 mwaka 2017.

Pamoja na kuwa kiasi cha dawa mpya za kulevya kilichokamatwa mwaka 2016 kilipungua lakini kumekuwa na ongezeko la nchi zinazotoa taarifa ya ukamataji wa dawa mpya za kulevya. Tahadhari imetolewa kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa mpya za kulevya hasa kwa wajidunga. Katika nchi nyingi ongezeko la dawa mpya za kulevya sokoni limehusishwa na vifo vya ghafla. Matumizi ya dawa mpya za kulevya magerezani limekuwa ni tatizo katika baadhi ya nchi za Ulaya, Amerika ya Kaskazini na Oceania.

Matumizi mabaya ya dawa tiba zenye asili ya Kulevya

Kumekuwa na ongezeko la matumizi holela ya dawa tiba zenye asili ya kulevya katika maeneo mbalimbali Duniani. Dawa tiba zenye asili ya kulevya zinazochepushwa kwa matumizi yasiyo ya kitiba ni tramadol, jamii ya valium, pethidine, morphine, phenobarbitone, ketamine, methadone, codeine buprenorphine na fentanyl.

Amerika ya Kaskazini dawa aina ya fentanyl inayopatikana kutoka vyanzo haramu huchanganywa na heroin pamoja na dawa nyingine na imekuwa chanzo kikubwa cha vifo vinavyotokana na kuzidisha dozi.

Katika nchi za Afrika ya Magharibi na Kaskazini pamoja na nchi za Mashariki ya Kati, kumejitokeza matumizi holela ya tramadol na dawa tiba nyingine ambazo hazidhibitiwi na mikataba ya kimataifa.

Kumekuwa na ukamatwaji mkubwa wa dawa tiba zilizokuwa zinauzwa kimagendo katika nchi za Afrika ya Magharibi, Kati na Kaskazini ambako dawa zilizokamatwa ni 87% ya dawa zote zilizokamatwa ulimwenguni katika mwaka 2016. Nchi za Bara la Asia ambazo kipindi cha nyuma zilikuwa zinakamata zaidi ya nusu ya dawa zote zilizokamatwa duniani zilikamata 7% ya dawa hizo katika mwaka 2016. Mwaka 2017 zaidi ya tani 150 ya dawa tiba zenye asili ya kulevya zilikamatwa duniani kote.

Ongezeko la ukamataji wa dawa tiba zinazosafirishwa kimagendo Afrika linatokana na matumizi holela ya tramadol ambayo haijawekwa kwenye udhibiti wa kimataifa. Tramadol ni dawa ya kuzuia maumivu ambayo huweza kusababisha uraibu pale inapotumika bila kufuata ushauri wa daktari. Utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO) unaonesha kuwa utegemezi huo unatokea dawa hiyo inapotumika kila siku kwa wiki chache. Tramadol hupelekwa katika masoko haramu ya Afrika ya Magharibi, Kati na Kaskazini na baada ya hapo kiasi kingine husafirishwa kwenda katika nchi za Mashariki ya Kati ambako kumekuwa na ongezeko la matumizi holela ya tramadol hasa kwa makundi ya watu wanaoishi katika mazingira hatarishi. Pamoja na kuwa tramadol inachepushwa kutoka vyanzo halali lakini tramadol nyingi iliyokamatwa katika kipindi cha 2012–2016 ilitoka kwenye maabara haramu za Bara la Asia

Ukamataji wa dawa za kulevya duniani

Bangi imeendelea kuwa dawa ya kulevya iliyokamatwa kwa kiasi kikubwa duniani. Mwaka 2017 tani 20,000 za bangi zilikamatwa na hekta 160,000 ziliteketezwa. Dawa zingine zilizokamatwa zaidi ni cocaine, dawa za kulevya jamii ya afyuni (opioids), dawa mpya za kulevya na dawa za kulevya jamii ya amfetamini (ATS) hususani metamfetamini. Kiasi kikubwa cha dawa za kulevya jamii ya afyuni kilichokamatwa kilikuwa ni heroin ikifuatiwa na dawa tiba zenye asili ya kulevya (pharmaceutical opioids) za tramadol na kiasi kidogo cha codeine, oxycodone na fentanyl.

Kiasi cha cocaine kilichokamatwa mwaka 2017 ni takribani tani 1,300 kiasi hiki kinakadiriwa kuwa ni ongezeko la 20% ya kiasi kilichokamatwa mwaka 2016. Hata hivyo ongezeko hili linatokana na ongezeko la kilimo cha mmea wa coca na utengenezaji wa cocaine katika miaka ya hivi karibuni.

Kiasi cha afyuni kilichokamatwa kiliongezeka kwa 13% mwaka 2017 ambacho kiliashiria ongezeko la uzalishaji wa morphine na heroin. Kulikuwa na ukamataji wa takribani tani 100 za heroin na morphine ambayo iliongezeka mara saba kwa kuwa na tani 65.

Katika dawa mpya za kulevya ongezeko zaidi lilikuwa kwenye dawa zinazotokana na mimea, ambazo ziliongezeka mara saba kutokana na ukamataji wa kratom. Mmea wa pili katika kundi hilo ulikuwa ni mirungi. Kiasi cha mirungi kilichokamatwa katika kipindi cha mwaka 2017 inakadiriwa kuwa tani 180.

Katika kundi la vipumbaza (sedatives and tranquillizers) iliyoongoza ilikuwa ni methaqualone (mandrax) ikifuatiwa na benzodiazepines wakati barbiturates ilikamatwa kwa kiwango kidogo. LSD pia ilikamatwa kwa upande wa vileta njozi (hallucinogens).

Udhibiti wa biashara ya dawa za kulevya mtandaoni

Kwa miaka ya hivi karibuni kumeibuka aina mpya ya biashara ya dawa za kulevya kwa kutumia mtandao na pesa za kidigitali. Julai 2017, majeshi ya polisi kutoka nchi mbalimbali yalishirikiana kudhibiti jukwaa maarufu la biashara ya dawa za kulevya mtandaoni liitwalo AlphaBay. Kabla ya kufungwa mtandao wa AlphaBay ulikuwa na wafuasi 250,000 kwa ajili ya biashara haramu ya dawa za kulevya na kemikali bashirifu. Mtandao huo ulikuwa na watumiaji wa dawa zaidi 200,000 na wauzaji 40,000. Pia jukwaa jingine lijulikana kama Hansa, ambalo lilikuwa ni jukwaa la tatu kwa ukubwa kwa biashara ya uhalifu mtandaoni lilivunjwa.

Makundi maalum yanayojihusisha na dawa za kulevya

Matumizi ya dawa za kulevya kwa wanawake

Idadi ya wanawake wanaotumia dawa tiba kama kilevi inazidi kwa kiasi kidogo idadi ya wanaume. Kwa upande mwingine wanaume wako juu zaidi katika matumizi ya dawa za kulevya kama bangi, cocaine na dawa za kulevya jamii ya afyuni (opiates). Wanawake wachache hujitokeza kwenye matibabu ya uraibu kwa wastani wa mwanamke mmoja kati ya watu watano. Hata hivyo, wanawake wenye uraibu wa dawa tiba hujitokeza kwa wingi zaidi

kwenye matibabu kuliko wanawake wenye uraibu wa dawa nyingine za kulevya. Wanawake wanaotumia dawa za kulevya huanza wakiwa na umri mkubwa kuliko wanaume, na huongeza kiwango cha vilevi wanavyovitumia kwa haraka zaidi ya wanaume “telescoping”. Wanawake wenye watoto huathiri familia zao kwa kiwango kikubwa zaidi kwa kushindwa kuwapa malezi bora watoto wao. Watoto wa wanawake hawa wako kwenye hatari kubwa ya kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya. Hali hii inatengeneza vizazi vya waraibu wa dawa za kulevya.

Wanawake na biashara ya dawa za kulevya

Wanawake pia wamekuwa wakishiriki katika mitandao ya biashara ya dawa za kulevya duniani. Hii inathibitishwa na wanawake waliofungwa katika nchi za Amerika ya Kusini na Afrika kwa kujihusisha na mitandao ya kimataifa ya biashara ya dawa za kulevya. Pia kuna taarifa za wanawake kuhusika katika kilimo cha afyuni (opium poppy) nchini Afghanistan na coca nchini Colombia. Takwimu zilizokusanywa na UNODC kutoka nchi mbalimbali kwa kipindi cha 2012–2016 zinaonyesha kati ya watu waliokamatwa kwa makosa yanayohusiana na dawa za kulevya 10% walikuwa ni wanawake.

Tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa wanawake wanaweza kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya pia wanajihusisha na matumizi ya dawa za kulevya. Tafiti nyingine zinaonyesha kuwa baadhi ya wanawake wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya ni waathirika wa biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu kwa ajili ya biashara ya ngono. Wengine wanaingizwa kwenye mtandao kutokana na unyonge wao, hofu na kwa kulazimishwa. Pia tafiti zimeonyesha kuwa wanawake wanaweza kukubali malipo kidogo kuliko wanaume na hivyo kuvutia mitandao ya biashara ya dawa za kulevya kutumia wanawake. Hata hivyo kuna taarifa kuwa baadhi ya wanawake wamejiingiza katika biashara ya dawa za kulevya kama chaguo lao bila kulazimishwa.

Wafungwa na matumizi ya dawa za kulevya

Matumizi ya dawa za kulevya yamebainika kuwepo miongoni mwa wafungwa katika magereza mbalimbali. Katika kipindi cha Mwaka 2018 ilikadiriwa kuwa, watu milioni 11 walikuwa wanaishi magerezani duniani kote. Idadi hii ilijumuisha wafungwa pamoja na Mahabusu. Kwa mujibu wa Taarifa ya hali ya dawa za kulevya Duniani ya mwaka 2018, inakadiriwa kuwa nusu ya wafungwa waliokuwa magerezani mwaka 2017 waliwahi kutumia dawa zakulevya katika maisha yao.

Miongoni mwa njia zinazotumika kutumia dawa za kulevya gerezani ni pamoja na kujidunga, kunusa na kuvuta. Wanaotumia njia ya kujidunga wapo kwenye hatari zaidi kutokana na kuchangia vifaa vya kujidungia. Hatua hii inasababisha kuwepo kwa maambukizi makubwa ya VVU na Homa ya ini aina B na C kwa watumiaji wa dawa za kulevya walioko gerezani. Hii huchangiwa pia na kutokuwepo kwa huduma za upunguzaji wa madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya katika magereza duniani. Huduma hii inapatikana katika nchi 6 tu Duniani. Kutokuwepo au kuwepo kwa huduma duni za afya kwa watumiaji wa dawa za kulevya walioko gerezani pia huchangia kuwepo kwa maambukizi makubwa ya magonjwa hayo.

Waraibu wa dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga wanaoacha kutumia dawa hizo wanapokuwa gerezani bila kupata huduma za ushauri nasaha juu ya kuzuia madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kuulevya, wana hatari kubwa ya kupata vifo vya ghafla vitokanavyo na kuzidisha dozi (overdose) pindi wanaporudia matumizi ya dawa hizo pale wanapotoka gerezani. Hii ni kutokana na mwili kutohimili kiwango cha dawa kinachoingia mwilini baada ya kutokutumia dawa kwa kipindi walichokuwa gerezani. Huduma za kupunguza madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya walioko gerezani ni muhimu ili kupunguza athari hizi.

Matibabu kwa waraibu

Kwa mujibu wa Taarifa ya dawa za kulevya Duniani ya mwaka 2019, watu milioni 35 wana matatizo yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya na wanahitaji matibabu. Hata hivyo, ni mtu mmoja tu kati ya watu saba wanaopatiwa matibabu hayo. Watu wanaotumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga sindano huathirika zaidi kiasi kuliko wasiojidunga. Utafiti unaolenga kupunguza athari za kiasi kwa wajidunga duniani ulionyesha kuwa nchi 79 pekee zimetokeleza mkakati wa kupunguza kuchangia sindano miongoni mwa wajidunga na tiba ya methadone. Aidha, nchi nne tu zilifikia daraja la juu la kutoa huduma hizo. Taarifa kuhusu uwepo wa huduma za kupima VVU na ushauri nasaha ni chache kwani nchi 34 ndizo zilidhibitisha kuwepo programu za upimaji wa VVU kwa wajidunga.

SURA YA PILI

2 UDHIBITI NA MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

Utangulizi

Katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya kuna nguzo kuu tatu. Nguzo hizo ni Kupunguza Upatikanaji wa Dawa za Kulevya, Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya, na Kupunguza Madhara yanayosababishwa na Matumizi ya Dawa za Kulevya.

Dawa za kulevya hususani bangi, heroin, mirungi, cocaine na viyeyushi (gundi na petroli) zimeendelea kuwa tatizo hapa nchini. Aidha, katika siku za karibuni kumekuwa na uchepushaji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya kama vile benzodiazepines, ketamine, tramadol na pethidine na kutumiwa kama vilevi. Halikadhalika, katika kipindi hicho kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu za uingizaji wa kemikali bashirifu ambazo pamoja na kuwa na matumizi halali huweza kuchepushwa na kutumika kutengeneza dawa za kulevya. Sura hii imejikita katika kuelezea mikakati iliyotekelezwa katika nguzo ya kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya nchini katika mwaka 2018.

Kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya

Mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, imeendelea kukabiliana na biashara na uzalishaji wa dawa za kulevya nchini. Jitihada zilizofanyika ni pamoja na kufanya operesheni mbalimbali za ukamataji, uteketezaji wa dawa za kulevya, kufuatilia uendeshaji wa kesi za dawa za kulevya na kutoa ushahidi mahakamani. Pia Mamlaka kwa kushirikiana na Mamlaka zingine za udhibiti imefanya kaguzi ili kuzuia uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya. Vilevile Mamlaka iliweza kubaini mitandao ya kihalifu ya ndani na nje ya nchi inayojihusisha na usafirishaji wa dawa za kulevya.

Mwenendo wa Biashara ya dawa za kulevya nchini

Biashara ya dawa za kulevya hufanyika kwa kificho na usiri mkubwa hivyo kuwa vigumu kupata takwimu sahihi za biashara hiyo. Hata hivyo, takwimu za ukamataji, idadi ya watuhumiwa na uteketezaji wa mashamba ya bangi vinaashiria kuwa biashara hii iliendelea kufanyika. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia dawa za kulevya na makosa mengine ya jinai (UNODC) mwaka 2018 Tanzania ilifanikiwa kudhibiti kiwango cha dawa aina ya heroin inayoingizwa nchini kutokea Afghanistan kwa 90%.

Hata hivyo Nchi yetu iliendelea kuwa njia ya kupitisha heroin kutoka Afghanistan kupitia Iran na Pakistan kwenda Afrika Kusini, nchi za Ulaya na maeneo mengine duniani kwa kiwango kidogo. Hii inadhihirishwa na kuwepo kwa watanzania waliokamatwa kwa tuhuma za usafirishaji wa dawa za kulevya katika nchi mbalimbali. Licha ya watanzania kujihusisha na biashara hii haramu, wapo pia raia wa kigeni kutoka nchi za Afrika Magharibi kama vile Nigeria na nchi za Asia zikiwemo Pakistan na Iran kukamatwa na dawa za kulevya kwenye Ukanda wa Pwani ya Tanzania. Mwenendo wa tatizo la biashara ya dawa za kulevya umeoneshwa hapa chini: -

Bangi



Bangi iliendelea kuzalishwa katika maeneo mbalimbali nchini hasa katika mikoa ya Mara, Tanga, Morogoro, Arusha, Kagera na Ruvuma. Kwa kipindi cha mwaka 2018 tani 24.3 za bangi zilikamatwa kiasi ambacho ni kidogo kulinganisha na tani 52.2 zilizokamatwa mwaka 2017. Hii pia inaonesha kuwa juhudi za kupambana na kudhibiti uzalishaji na usambazaji wa dawa hii una mafanikio. Pia, takwimu za ukamataji zinaonesha kuwa idadi ya watuhumiwa waliojihusisha na biashara ya bangi mwaka 2018 ilikuwa 10,061 ikilinganishwa na watuhumiwa 11,528 waliohusishwa na biashara ya dawa hiyo mwaka 2017. (*Rejea Jedwali Na.1 na Kielelezo Na.1*).

Mirungi




Mwaka 2018 biashara ya mirungi iliendelea kufanyika ambapo jumla ya tani 8.97 za dawa hii zilikamatwa. Pia mwaka huo, kulikuwa na watuhumiwa 1,186 waliojihusisha na biashara hiyo, ambayo ni idadi ndogo ikilinganishwa na idadi ya watuhumiwa katika miaka ya karibuni. (*Rejea Jedwali Na.1 na Kielelezo Na 1*).

Jedwali Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2008-2018

Mwaka	Bangi (Tani)	Mirungi (Tani)
2008	76.40	5.33
2009	56.20	22.90
2010	4.03	3.69
2011	17.30	0.10
2012	48.70	6.22
2013	85.80	12.82
2014	81.30	15.74
2015	22.01	16.60
2016	68.23	21.64
2017	52.19	67.81
2018	24.30	8.97

Kielelezo Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2008 - 2018




Kutokana na takwimu hizo hapo juu, kiasi cha bangi kilichokamatwa kilianza kupungua kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka 2018. Halikadhalika, kiasi cha mirungi kilichokamatwa mwaka 2018 kilikuwa kidogo kulinganisha na kiasi kilichokamatwa mwaka 2017. Hali hii inatokana na maboresho ya Sheria ya Mwaka 2017 ambayo yaliongeza adhabu kwa wasafirishaji, na kupunguza viwango vya dhamana. Pia, kuimarika kwa juhudi za ukamataji na uteketezaji wa mashamba ya bangi na mirungi nchini.

Jedwali Na. 2: Idadi ya watuhumiwa wa Bangi na Mirungi waliokamatwa kati ya mwaka 2008-2018

Mwaka	Bangi	Mirungi
2008	5,670	468
2009	3,382	365
2010	11	26
2011	39	100
2012	5,548	847
2013	1,547	581
2014	11,918	1,650
2015	13,275	1,780
2016	17,889	2,397
2017	11,528	1,797
2018	10,061	1,186

Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa idadi ya watuhumiwa waliokamatwa kwa kujihusisha na Bangi na Mirungi nchini kati ya Mwaka 2008 - 2018



Kielelezo Na. 2 kinaonesha idadi ya watuhumiwa waliojihusisha na biashara na kilimo cha bangi na mirungi nchini katika mwaka 2018 ilipungua kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na miaka iliyotangulia. Hali hii inaendana na kiasi kidogo cha dawa za kulevya kilichokamatwa katika mwaka 2018.

Heroin

Mwaka 2018 jumla ya kilo 16.94 za heroin zilikamatwa nchini zikiwahusisha watuhumiwa 744. (Rejea Jedwali Na.2 na Kielelezo Na.2).


Cocaine

Mwaka 2018 biashara ya cocaine iliendelea kuwepo katika maeneo mbalimbali nchini. Hii inadhihirishwa na kukamatwa kwa kilo 8.9 za cocaine zikiwahusisha watuhumiwa 156 (*Rejea Jedwali Na.3 na Kielelezo Na.3*).


Jedwali Na. 3: Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2008-2018.

Mwaka	Cocaine (Kg)	Heroin (Kg)
2008	3.50	3.70
2009	4.39	9.00
2010	62.97	185.80
2011	128.00	264.26
2012	151.00	260.00
2013	4.00	36.00
2014	45.00	400.00
2015	17.79	64.75
2017	18.52	42.26
2017	4.14	185.56
2018	8.90	16.94

Kielelezo Na. 3: Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2008 - 2018




Kielelezo Na. 4: Mwenendo wa kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2008 - 2018




Jedwali Na. 4: Idadi ya watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa nchini kati ya Mwaka 2008 - 2018.

Mwaka	Cocaine	Heroin
2008	251	203
2009	108	122
2010	8	15
2011	30	20
2012	138	400
2013	20	75
2014	351	584
2015	281	474
2016	263	716
2017	243	1005
2018	156	744

Kielelezo Na. 5: Idadi ya watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa nchini kati ya Mwaka 2008 - 2018



Kielelezo Na. 6: Mwenendo wa idadi ya watuhumiwa waliokamatwa wakijihusisha na Heroin na Cocaine kati ya Mwaka 2008 - 2018



Udhibiti wa Kemikali bashirifu na Dawa tiba zenye asili ya kulevyva

Udhibiti wa kemikali bashirifu ni muhimu katika kuzuia uchepushwaji wa kemikali hizo kutumika kama malighafi au kutumika katika mchakato wa kutengeneza dawa za kulevyva. Udhibiti huo umeendelea kufanyika kwa mujibu wa Sheria zilizopo ikiwa ni pamoja na Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyva. Udhibiti huo umefanyika kupitia njia za ukaguzi, kutoa vibali vya kuingiza au kusafirisha nje ya nchi kemikali bashirifu, pamoja na kufanya uchunguzi wa kimaabara ili kubaini aina ya kemikali zinazokamatwa au kutiliwa mashaka.

Aidha, zipo dawa tiba zenye asili ya kulevyva kama vile pethidine, ketamine, morphine, tramadol, na nyinginezo zinazoweza kuchepushwa na kutumika kama mbadala wa dawa za kulevyva pia udhibiti wa dawa hizo ni muhimu katika vita dhidi ya dawa za kulevyva.

Katika kipindi cha Mwaka 2018, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na dawa za kulevyva kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za udhibiti ilifanya ukaguzi ambao ulikwenda sambamba na kutoa elimu ya udhibiti kwenye jumla ya maeneo 175 ambayo kati ya hayo maduka ya dawa yalikuwa 145 na hospitali 11, makampuni yanayojihusisha na kemikali bashirifu 30. Ukaguzi huo ulifanyika katika mikoa ya Dodoma, Iringa, Arusha, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Tanga, Morogoro, Pwani, Mwanza, Shinyanga na Mara.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwepo kwa mtandao unaojihusisha na uingizaji haramu wa dawa aina ya pethidine katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro na hivyo kufanikisha kukamata watuhumiwa sita ambao walifikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua za kisheria. Halikadhalika, katika kipindi hicho Mamlaka kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za udhibiti ilifanikiwa kukamata dawa ya kikohozi aina ya *coldril syrup* kiasi cha lita 10,000 zenye kiambata pungufu cha kemikali bashirifu aina ya *pseudoephedrine* katika kampuni mojawapo ya kutengeneza dawa za binadamu nchini. Uchunguzi ulibaini kwamba upungufu wa kiambata cha kemikali aina ya pseudoephedrine ulitokana na uchepushwaji wa kemikali hiyo kiasi cha kilo 6.36.

Udhibiti wa Kemikali bashirifu kupitia mfumo wa kielektroniki

Sambamba na mifumo mingine iliyopo ya kisheria ya udhibiti wa kemikali bashirifu, Mamlaka ilifuatilia mienendo ya uingizaji nchini wa kemikali bashirifu kupitia mifumo ya kielektroniki kwa kubadilishana taarifa na Mamlaka nyingine za udhibiti duniani. Katika kipindi cha mwaka 2018, Mamlaka ilizuia kuingizwa nchini kiasi cha kemikali tani 33.2 ambazo ziilikuwa ziingizwe nchini kinyume cha Sheria. Miongoni mwa ukiukwaji wa taratibu zilizobainika ni pamoja na waagizaji wa kemikali kutumia majina ya kampuni nyingine bila ridhaa ya kampuni husika.

Uteketezaji wa dawa za kulevya

Jumla ya magunia 328 ya bangi yenye uzito wa tani 6.7 yaliyokamatwa katika operesheni za kupambana na dawa za kulevya wilayani Arumeru mkoani Arusha yaliteketezwa. Pia kilo tano na gramu 250 za heroin ziliteteketezwa mkoani Kilimanjaro.

Kesi za dawa za kulevya

Katika kipindi cha mwaka 2018 jumla ya kesi 7,593 zikiwa na jumla ya watuhumiwa 10,979 zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali nchini. Katika jumla ya kesi 7,174 zilizowahusisha watuhumiwa 11,045 ziliendelea kusikilizwa katika hatua mbalimbali. Idadi ya kesi na watuhumiwa katika kipindi hicho zimeainishwa katika jedwali na 5

Jedwali Na. 5: Kesi zilizofikishwa mahakamani mwaka 2018

Aina ya dawa	Idadi ya kesi zilizoripotiwa	Kesi zilizofikishwa mahakamani	Kesi zilizopata mafanikio	Kesi zilizoshindwa
Dawa za kulevya za viwandani				
Heroin	309	253	46	10
Cocaine	72	65	6	1
Mandrax	1	1	0	0
Bangi iliyosindikwa	1	1	0	0
Jumla	383	320	52	11
Dawa za kulevya za mashambani				
Bangi	6,237	5,919	482	110
Mirungi	1,025	935	76	17
Jumla	7,210	6,854	558	127

Katika kipindi cha mwaka 2018 jumla ya kesi 748 zilitolewa maamuzi mahakamani, kati ya hizo Jamhuri ilishinda jumla ya kesi 610 ambayo ni 81.6% na kupoteza jumla ya kesi 138 ambayo ni 18%. Mafanikio hayo yametokana na kuimarika kwa mifumo ya upelelezi na uendeshaji wa mashtaka.

Jedwali Na. 6: Watuhumiwa waliofikishwa mahakamani mwezi Januari - Desemba, 2018

Aina ya dawa	Idadi ya watuhumiwa		kesi zilizo mahakamani		Waliopatikana na hatia		Wasiopatikana na hatia	
	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke	Me	Ke
Watuhumiwa wa dawa za kulevya za viwandani								
Heroin	692	52	629	47	51	4	12	1
Cocaine	118	38	103	38	12	0	3	0
Mandrax	1	0	1	0	0	0	0	1
Bangi iliyosindikwa	1	0	1	0	0	0	0	0
Jumla	812	90	734	85	63	4	15	2
Watuhumiwa wa dawa za kulevya za mashambani								
Bangi	9,208	853	8372	776	681	63	155	14
Mirungi	959	227	872	206	71	17	16	4
Jumla	10,167	1,080	9,244	982	752	80	171	18
JUMLA KUU	10,979	1,170	9,978	1,067	815	84	186	19

Kulingana na takwimu za mwaka 2018 zilizoainishwa katika jedwali Na. 6 imeonekana kuwa wanawake pia wamekuwa wakijihusisha na biashara ya dawa za kulevya ambapo kati ya watuhumiwa 10,979, wanawake walikuwa 1,170 ambao ni sawa na 10.6%.

SURA YA TATU

3 KUPUNGUZA UHITAJI (MATUMIZI) NA MADHARA YANAYOSABISHWA NA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA

Sura hii ni mwendelezo wa sura ya pili ambazo kwa pamoja zinaonesha jitihada zilizofanyika katika kukabiliana na dawa za kulevya nchini. Aidha, sura hii imejikita katika kuelezea mikakati iliyotekelezwa katika nguzo ya pili na ya tatu zinazotekelezwa sambamba ambazo ni kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya pamoja na kupunguza madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya.

Tatizo la Uhitaji (matumizi) wa dawa za kulevya nchini

Katika kipindi cha mwaka 2018 matumizi ya dawa za kulevya yaliendelea kuwepo nchini. Hali hii inadhihirishwa na uwepo wa watumiaji waliojitokeza kutafuta tiba, huduma za utengemao na misaada mbalimbali katika vituo vya kutolea huduma za afya, nyumba za upataji nafuu na asasi za kiraia zinazotoa huduma kwa watumiaji wa dawa za kulevya. Dawa zinazotumiwa zaidi nchini ni pamoja na bangi, mirungi, heroin, cocaine na dawa tiba zenye asili ya kulevya mfano valium, tramadol na pethidine. Aidha, dawa zinazotokana na mimea inayostawi hapa nchini kama bangi na mirungi hutumika katika mikoa yote. Heroin na kiasi kidogo cha cocaine zimekuwa zikitumiwa zaidi kwenye miji mikubwa. Dawa hizo hutumika kwa kificho katika maeneo mbalimbali nchini.

Sababu zinazochangia matumizi ya dawa za kulevya

Matumizi ya dawa za kulevya huchangiwa na sababu mbalimbali. Miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na msukumo rika, malezi duni, migogoro ya kifamilia, upatikanaji rahisi wa baadhi ya dawa za kulevya, mazingira magumu ya kazi kama vile, uchimbaji wa madini, ukuli na ukahaba, uelewa mdogo juu ya madhara ya dawa za kulevya katika jamii. Sababu nyingine ni ukosefu wa ajira utandawazi, upungufu wa stadi za maisha na tabia ya udadisi inayojitokeza zaidi katika kipindi cha kutoka ujana kwenda utu uzima (miaka 12 hadi 21). Aidha, pamoja na kuhalalishwa kwa bidhaa za pombe na tumbaku tafiti zinaonesha kuwa bidhaa hizo huchochea pia matumizi ya dawa nyingine za kulevya.

Madhara yanayosababishwa na matumizi na biashara ya dawa za kulevya

Kiafya

Matumizi ya dawa za kulevya yanaweza kusababisha magonjwa mbalimbali yakiwemo uraibu, magonjwa ya akili, magonjwa ya ini, mapafu/kifua kikuu, pamoja na magonjwa ya moyo. Aidha, matumizi ya dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga huchangia kuenea kwa maambukizi ya VVU, virusi vya homa ya ini aina B na C miongoni mwa watumiaji na jamii kwa ujumla. Matumizi ya kiwango kikubwa cha dawa za kulevya kuliko alichozoea mtumiaji, husababisha vifo vya ghafla hasa kwa wajidunga.

Watumiaji wa dawa za kulevya hasa wanawake wajawazito wamekuwa wakijifungua watoto wenye utegemezi wa dawa za kulevya na mara nyingi watoto wanaozaliwa wamekuwa na matatizo mengine ya kiafya yakiwemo ya akili na kuathiri ukuaji. Madhara mengine ya

kiafya ni pamoja na saratani, sonona, kukosa usingizi, kuoza meno na vidonda kwenye mfumo wa chakula.

Kiuchumi.

Matumizi na biashara ya dawa za kulevya huathiri ukuaji wa uchumi wa nchi kwa namna mbalimbali. Athari hizo ni pamoja na kudhoofisha afya za watumiaji ambao asilimia kubwa ni nguvu kazi ya Taifa hivyo kuathiri uzalishaji. Matumizi ya dawa hizo huathiri walio kwenye ajira katika sekta mbalimbali zinazochochea ukuaji wa uchumi kama vile kilimo na viwanda kwa kuwa ufanisi wao hupungua kutokana na utoro na kupungua kwa umakini na baadhi hupoteza ajira. Aidha, watumiaji walio nje ya ajira hushindwa kupata ajira kutokana na uraibu.

Biashara ya dawa za kulevya huathiri ukuaji wa uchumi kwa kuharibu mzunguko wa fedha. Athari hizo ni pamoja na mfumuko wa bei ambao husababishwa na fedha haramu zinazotokana na biashara hiyo, Wenye fedha haramu zinazotokana na biashara ya dawa za kulevya huweza kuhodhi sehemu kubwa ya rasilimali za jamii kama vile ardhi na kuwaacha wenye kipato cha kawaida bila chochote. Wafanyabiashara wa dawa za kulevya hujihusisha na vitendo vya rushwa ili kuchukua fursa nyingi za kibiashara hivyo, huwaacha wawekezaji wenye kipato cha kawaida bila fursa. Aidha, biashara ya dawa za kulevya huambatana na utakatishaji wa fedha haramu zinazotokana na dawa za kulevya ambapo huathiri ukuaji wa uchumi.

Vilevile, gharama za uhibitaji zikiwemo utoaji wa elimu kwa umma, uteketezaji wa mashamba ya bangi, uendeshaji wa kesi, kuwatunza wafungwa magerezani na kuwatibu watumiaji huongeza mzigo kwa taifa na jamii kwa ujumla ambapo bajeti ya shughuli hizo ingeweza kutumika kuboresha sekta muhimu kama vile afya, elimu na viwanda.

Kijamii

Madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya husababisha umaskini, familia kutengana, uwepo wa watoto wa mtaani, utoro shuleni, ongezeko la wazazi wanaotelekeza watoto kwa kushindwa kutimiza majukumu yao kutokana na matumizi ya dawa za kulevya, pamoja na mmomonyoko wa maadili. Unyanyapaa kwa watumiaji na kuwafanya wakose huduma za kijamii na haki zao.

Kiusalama

Fedha zinazopatikana kutokana na biashara ya dawa za kulevya hutumika kufadhili vikundi vya kihalifu ikiwemo ugaidi. Wengi wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya hujihusisha na uhalifu mwingine kama biashara ya binadamu ambapo huwaweka watu rehani, kufanya biashara haramu ya silaha na kuendesha madanguro. Maeneo ambayo biashara na matumizi ya dawa za kulevya vimeshamiri hukosa usalama na kutawaliwa na vitendo vya uporaji, wizi, mapigano, utekaji na hata mauaji. Waendeshaji wa mitambo na vyombo vya moto waliotumia vilevi huweza kusababisha ajali na kusababisha uharibifu wa mali, ulemavu na vifo vinavyozuilika kwao wenyewe au kwa watu wengine.

Kisiasa

Wafanyabiashara wa dawa za kulevya hujingiza kwenye siasa na kupata uongozi hivyo kufanya biashara hiyo kushamiri. Aidha, wafanyabiashara wa dawa za kulevya huweza kuwezesha mapinduzi au kuondoa tawala halali hivyo kuvuruga demokrasia. Vilevile, wafanyabiashara hao wanaweza kufadhili chaguzi na kuwaweka watu wao madarakani ili

kulinda biashara zao. Hali hii hufanya biashara na matumizi ya dawa za kulevya kukua na kuathiri mustakabali wa jamii husika.

Kimazingira.

Ukataji miti kuandaa mashamba ya bangi kwenye misitu au milima husababisha kukauka kwa vyanzo vya maji, mmomonyoko wa udongo, kutoweka kwa baadhi ya viumbe hai na uoto wa asili, ukame na njaa. Uharibifu huu umejidhirisha katika baadhi ya safu za milima ya Uluguru, Usambara, Udzungwa na maeneo ya Arumeru. Watumiaji wa dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga wamekuwa wakitupa ovyo sindano na kusababisha uchafuzi wa mazingira katika maeneo wanayotumia kujidungia kama vile fukwe za bahari, vituo vya daladala, viwanja vya michezo na maeneo mengine mitaani.

Kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya

Mamlaka kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inatoa elimu juu ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevya kwa makundi mbalimbali ya kijamii ili wasijihusishe na matumizi ya dawa hizo hatari. Elimu hii hutolewa kupitia vyombo vya habari, machapisho, maonesho ya kitaifa, semina na makongamano. Elimu ya dawa za kulevya ilitolewa wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kupambana na Dawa za Kulevya Duniani yaliyoadhimishwa kitaifa mkoani Iringa, Juni 2018. Elimu pia ilitolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari, kwenye makongamano ya kutimiza miaka 100 ya uskauti nchini, kamati za ulinzi na usalama, vyuo vya kawaida na vyuo vikuu na kwenye shule za msingi na sekondari katika mikoa mbalimbali.

Elimu ilindelea kutolewa na asasi mbalimbali katika shule za Msingi, Sekondari na vyuoni na kuzisimamia, kuanzisha klab mpya na za kudumu mashuleni. Elimu ya utambuzi wa tabia, unasihi na kurekesha tabia kwa vijana waraibu wanaoendelea kupata nafuu, kutoa elimu katika seminary ya mapadri Tabora, pia ilitolewa kwenye mbio za mwenge na kwenye vyombo vya habari. Mafunzo ya utengenezaji mkaa mbadala kwa vijana yalitolewa, huduma za vikoba, mijadala juu ya mahusiano ya dawa za kulevya na VVU, kundwa kwa timu ya uelimishaji rika, walioko mitaani, kufanya bonanza la michezo mashuleni, na vituo vya kusaidia vijana na jamii iliyoathirika na matumizi ya dawa za kulevya.

Asasi hizo zimeendelea kutoa elimu katika matamasha na makongamano mbalimbali katika mikoa tofauti tofauti, baadhi ya asasi hizo ni Kibwena Community Development (KCD), International Organization of Good Templars (T-IOGT), Gulukakwalala Youth Environment Group, Youth Achiverment Village in Tanzania (YAVT), Elimisha Initiative, Matumaini Group, Lake Tanganyika Development and Relief Organization, Kiona youth Coordinates (KYCo), NURGET Development Tanzania, Kimara Peer Educators and Health Promoters Trust Fund, Tandika Youth And Handcraft Group (TAYOHAG), Nazareth Kwaya, Anti Alcoholism and Drug Addiction Organization (AADA0) na Next Generation Keepers.

Aidha, Mamlaka huratibu uandaaji na kusimamia utekelezaji wa miongozo ya utoaji elimu katika makundi mbalimbali ya kijamii pamoja na kujumuisha suala la dawa za kulevya katika mitaala ya ngazi mbalimbali za elimu. Mamlaka pia huwezesha wadau mbalimbali kutekeleza jukumu hili kwa kuwajengea uwezo.

Mamlaka ilifanikiwa kutoa elimu ya namna bora ya kudhibiti uchepushwaji wa kemikali bashirifu ili kuzuia kuchepushwa. Elimu hiyo ilitolewa kwa wadau mbalimbali wanaojihusisha na biashara ya kemikali bashirifu ambapo jumla ya wadau 183 walipewa

elimu, wakiwemo wasafirishaji 54, wasimamimizi wa kemikali 109 na waingizaji na wasambazaji wakubwa wa kemikali 20.

Kupunguza madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya

Kupunguza madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya ni nguzo ya tatu muhimu katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya nchini. Katika nguzo hii Mamlaka imekuwa ikitoa elimu ya afya kwa watumiaji wa dawa za kulevya, kuandaa miongozo, kuratibu na kuanzisha vituo vya matibabu ya uraibu kwa kutumia tiba ya Methadone hasa kwa waathirika wa dawa aina ya heroin na kusimamia nyumba za upataji nafuu.

Maambukizi ya VVU, virusi vya homa ya ini na ugonjwa wa kifua kikuu kwa watumiaji wa dawa za kulevya huwa na kiwango kikubwa hivyo hupatiwa huduma ili kupunguza maambukizi haya kuenea kwenye jamii. Kulingana na takwimu za mwaka 2014 kiwango cha maambukizi ya VVU kwa watumiaji wa dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga ilikuwa ni 35% wakati katika jamii kwa ujumla kiwango cha maambukizi kilikuwa 5.8%.

Jitihada zinazofanyika kuhakikisha watumiaji wa dawa za kulevya wanapata huduma za matibabu kwa ajili ya kupunguza maambukizi ya maradhi miongoni mwao na jamii inayowazunguka, huduma za unasihi na stadi za kazi hivyo kuboresha maisha yao na kuwafanya waweze kujitegemea. Huduma hizi hutolewa katika asasi, nyumba za upataji nafuu (sober houses), kliniki za methadone na kwenye baadhi ya vituo vya afya.

Tiba ya methadone

Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na wadau wa maendeleo imeratibu, uanzishaji, na uendeshaji wa huduma ya tiba ya methadone kwa waathirika wa dawa ya kulevya aina ya Heroin. Katika kipindi cha mwaka 2018 Mamlaka ilifanikiwa kufikisha huduma ya tiba ya methadone kwa mara ya kwanza kwa waraibu wa mkoa wa Mwanza katika hospitali ya Sekou Toure.

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2011 hadi kufikia mwaka 2018 huduma hizi zimekuwa zikitolewa bila malipo katika vituo vya afya vya Muhimbili, Mwananyamala, Temeke, Mbeya, na Mwanza. Hadi Desemba 2018 jumla ya waraibu wa dawa za kulevya 6,204 walipatiwa huduma hii ikiambatana na huduma nyingine zinazotolewa kwa waraibu wa dawa za kulevya.

Hata hivyo kumekuwa na ongezeko la waraibu waliosajiliwa katika tiba ya Methadone kwa 69.4% kutoka waraibu 4,307 mwaka 2017 hadi kufikia 6,204 mwaka 2018. Aidha, wanawake waliojitokeza kupata tiba ya methadone ni wachache ukilinganisha na idadi ya wanaume. Pamoja na kwamba idadi ya wanawake wanaotumia dawa za kulevya ni wachache ukilinganisha na wanaume, bado idadi ya wanawake wanaojitokeza kupata huduma ya matibabu ni ndogo sana.

Mamlaka imesimamia na kuratibu utafiti wa matumizi ya dawa ya methadone nyumbani badala ya waraibu kuhudhuria katika vituo vya kupatiwa dawa kila siku, ili kusaidia waraibu kupata huduma kwa urahisi. Mamlaka pia ina ratibu mafunzo mbalimbali kwa watoa huduma za afya ili kuwajengea uwezo katika utoaji huduma.

Methadone ni tiba inayosaidia kupunguza utegemezi wa dawa ya kulevya aina ya heroin, hata hivyo uchunguzi na matibabu ya magonjwa mengine kama vile; maambukizi ya VVU, homa ya ini aina ya B na C, kifua kikuu na kifua kikuu sugu pamoja na magonjwa ya zinaa hufanyika katika vituo hivyo.

Vilevile, huduma za magonjwa ya akili, uzazi kwa mama na mtoto na huduma nyingine za kijamii hutolewa katika vituo hivyo. Huduma hii imesaidia kupunguza vifo vya ghafla kutokana na kuzidisha dozi ya dawa aina ya heroin. Huduma ya methadone inasaidia pia kupunguza matendo ya kihalifu, uvunjifu wa amani na kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

Kuwaandaa waraibu kuanza kutumia methadone

Asasi ziliendelea kutoa huduma ya kuwaandaa waraibu kwa ajili ya kuanza kupata huduma ya Methadone, waliweza kwenda kwenye vijiwe mbali mabali kuwapatia huduma ya unasihi, elimu ya dawa za kulevya, kuwapima maambukizi ya kufua kikuu, VVU na kuwapa elimu ya kujinga salama ili wasiweze kupata magonjwa ambukizi, Asasi zilizotoa huduma hizo ni MUKIKUTE, Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA), Youth Volunteers Against Behaviours (YOVARIBE) na Youth Counseling and Rehabilitation (YCR).

Jedwali Na. 7: Waraibu Waliopata Huduma ya Methadone Tangu 2011 - 2018

Suala	Wanaume	Wanawake	Jumla
Idadi ya Waraibu waliosajiliwa toka kuanzishwa kwa Huduma.	5,798	406	6,204
Idadi ya Waraibu waliokuwa wanatumia Methadone hadi Desemba 2018	3,723	267	3,990
Waliokutwa na maambukizi ya VVU	422	161	583
Waliokutwa na maambukizi ya Homa ya Ini C	659	74	733
Waliokutwa na maambukizi ya Homa ya Ini B	470	72	542
Waliokutwa na ugonjwa wa Kifua kikuu.	340	48	388

Huduma ya upataji nafuu kwa watumiaji wa dawa za kulevya (Sober House)

Waraibu wa dawa za kulevya waliendelea kupata huduma za upataji nafuu katika nyumba maalum za upataji nafuu (sober house) katika kipindi cha mwaka 2018. Katika kipindi hicho nyumba za upataji nafuu zimeongezeka kutoka nyumba 24 mwaka 2017 hadi kufikia nyumba 30. Aidha, nyumba hizi zinapatikana katika mikoa ya Tabora, Tanga, Dar es salaam, Dodoma, Kagera, Iringa, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Mwanza, na Pwani. Vilevile Mamlaka iliendelea kuratibu uanzishaji na kusimamia uendeshaji wa nyumba hizo kwa

kutumia Mwongozo wa Namna ya Kuanzisha na Kuendesha Nyumba za Upataji Nafuu (The Guideline Manual of Standards for Establishing and Operating Sober Houses in Mainland Tanzania). Nyumba hizi zinaendesha na asasi zisizo za kiserikali ambapo waraibu wa dawa za kulevya za aina mbalimbali husaidiwa kuachana na matumizi ya dawa za kulevya kwa kutumia unasihi bila kutumia dawa yoyote.

Baadhi ya nyumba hizo ni Tabora sober house, Gift of Hope Foundation, Kipepeo Foundation-South Beach Sober House, Courage on Recovery Foundation, Chagamoto ni Matumaini, People with Drug Dependence Relief Foundation (PEDDEREF), Sobriety Forever Rehabilitation Centre, Foundation For Alleviation Of Drug Addiction And Suffering (FADAS), Morogoro Recovery Community Tanzania (MRC), Drug Free Tanzania (The Ties that bind us together recovery), Drug Free Tanzania (Right Way Recovery House), Tanzania Sobriety and Change Foundation (TSCF), Pillimisanah Foundation, Stay Clean Foundation-(Goodwill recovery centre) na The Light of Miracle Organization.

Huduma katika vituo vya afya

Vituo vya kutolea huduma za afya vya wilaya, rufaa mkoa na rufaa kanda vinatoa huduma kwa waraibu wa dawa za kulevya. Katika mwaka 2018, jumla ya waraibu 12,010 walihudumiwa katika vituo hivyo nchini.

SURA YA NNE

4 CHANGAMOTO, HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA MIPANGO YA BAADAYE

Udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevywa kwa mwaka 2018 ulikuwa na mafanikio licha ya kuwepo kwa matatizo na changamoto mbalimbali. Sura hii imeainisha changamoto na mikakati iliyojiwekea Mamlaka katika kuongeza ufanisi wa udhibiti wa dawa za kulevywa nchini.

Changamoto na hatua zilizochochuliwa

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho zipo changamoto mbalimbali zilizojitokeza. Hata hivyo, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wengine ilifanya jitihada mbalimbali katika kukabiliana na changamoto hizo.

- i. Katika kukabiliana na changamoto ya ukubwa wa mipaka na ukanda mrefu wa bahari ya Hindi unaosababisha udhibiti wa dawa za kulevywa kuwa mgumu, Mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ilitambua bandari bubu zinazotumika kuingiza dawa hizo na kuimarisha doria kwenye maji bahari na mipaka ya nchi kavu.
- ii. Ili kubaini mbinu mbalimbali zinazotumiwa na wafanyabiashara wa dawa za kulevywa ambazo hubadilika mara kwa mara kutokana na kukua kwa teknolojia yalitolewa mafunzo kwa watumishi wanaojihusisha na udhibiti wa dawa za kulevywa ili kuwaongezea uwezo wa kutambua mbinu hizo
- iii. Katika kukabiliana na ongezeko la uzalishaji wa dawa mpya za kulevywa za viwandani zisizodhibitiwa na sheria zinazotengenezwa na kemikali bashirifu. Mamlaka kwa kushirikiana na mamlaka zingine za udhibiti iliendelea kufanya ukaguzi maeneo mbalimbali kama vile kwenye maduka, viwanda, kampuni za usafirishaji vifurushi na maeneo ya starehe.
- iv. Katika kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya huduma za matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevywa Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wengine walifungua kituo cha tiba ya methadone mkoani Mwanza na kuongeza idadi ya vituo hivyo na kufikia sita. Vilevile, nyumba za upataji nafuu ziliongezeka kutoka 24 mwaka 2017 hadi 30 mwaka 2018
- v. Kutokana na changamoto ya unyanyapaa na uelewa mdogo juu ya tatizo la dawa za kulevywa, elimu ilitolewa kwa jamii ili wajiepushe na matumizi na biashara ya dawa za kulevywa, kupunguza unyanyapaa kwa waraibu ikiwa ni pamoja na kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya dawa za kulevywa
- vi. Ukosefu wa mfumo rasmi wa kuwajengea uwezo wa ujasiriamali wanaoacha matumizi ya dawa za kulevywa baada ya tiba,

vii. Kutokana na changamoto ya kukinzana kwa sheria ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya na nchi nyingine, Tanzania imeendelea kushirikiana na nchi nyingine kupitia mikataba ya kimataifa na ya kikanda kukabiliana na changamoto hii

viii. Ili kukabiliana na changamoto ya ongezeko la matumizi mabaya ya dawa tiba zenye asili ya kulevya, Mamlaka kwa kushirikiana na mamlaka zingine za udhibiti zimeendelea kuimarisha ukaguzi na kuchukua hatua kwa wanaokiuka taratibu zilizoainishwa na sheria za udhibiti.

Mipango ya baadaye

Mamlaka imepanga kuongeza udhibiti na mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya kwa kufanya yafuatayo:

- **Elimu juu ya athari za matumizi na biashara ya dawa za kulevya.**

Kuongeza nguvu zaidi katika kutoa elimu kwa umma juu ya madhara yanayotokana na matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Mamlaka kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itajielekeza katika kuongeza utoaji wa elimu ili kupunguza kundi la wanaotaka kujiingiza katika kutumia dawa za kulevya na kwa wale ambao wameshaanza basi kuwaelekeza vituo ambavyo wanaweza kupata tiba.

- **Mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevya**

Mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola pamoja na jamii itajielekeza katika kuboresha mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevya ikiwemo kushirikisha taasisi na vyombo vingine vya kimataifa ili kuleta tija. Mapambano hayo yatajikita zaidi katika kuhakikisha dawa za kulevya haziingizwi nchini na zile ambazo zimeshapenya hazisambazwi mitaani kwa kuwakamata wahusika na dawa hizo. Vilevile Mamlaka itaimarisha uchunguzi wa sayansi jinai ikiwa ni pamoja na kuanzisha kwa maabara yenye uwezo wa kufanya tafiti na utambuzi wa dawa mpya na zilizopo sokoni.

- **Utoaji wa tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya**

Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itaendelea kutia nguvu juhudi za upanuzi wa huduma za tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya na kuhakikisha huduma hizi zinawafikia wahusika karibu na maeneo yao ili kuongeza ushiriki wao katika kupata huduma hizo. Upanuzi wa huduma hizo utahusisha pia kuweka dirisha maalum katika hospitali za rufaa za mikoa yote nchini litakalokuwa linatoa huduma kwa waathirika wa dawa za kulevya.